TUSONGE - CDO NGUVU yetu

Oktoba-Desemba 2014 Toleo la 3 uk. 1

WASEMAVYO WALENGWA WA TUSONGE KATIKA MAHOJIANO YAO NA AFISA UFUATILIAJI NA AFISA KAZI JAMII

UTANGULIZI

TUSONGE ni shirika la kijamii lililoko mkoani Kilimanjaro na linajihusisha na shughuli za kijamii hasa kwenye eneo la kuwezesha wanawake na vijana wa makundi ya pembezoni kujikwamua kiuchumi.

Shirika hili ambalo linafanya kazi ya kutoa elimu ya ujasiriamali na kuferejisha masuala ya haki za binadamu, jinsia, Uongozi na Afya ya uzazi na UKIMWI liko katika jamii yetu tangia 2011.

Shirika la TUSONGE linafanya kazi zake kwa kuheshimu mbinu shirikishi na zaidi kuona kuwa jamii inao uwezo mkubwa sana wa kuleta mabadiliko yao wenyewe. Kwa kulitambua hilo TUSONGE imeweka mpango wa kutoa elimu ya ujasiriamali ili kuweza kunoa stadi za wajasiriamali hao na pia kuweza kuwapa nafasi ya kufikiri zaidi katika utendaji ili kuleta tija zaidi katika biashara zao kwa kulenga kuboresha ustawi wa familia zao na za jamii inayowazunguka. Yapo mabadiliko chanya ambayo yameshaweza kujitokeza katika ubia huu na kuheshimu sauti za jamii na michango yao. Mahojiano maalumu na baadhi ya wadau yalifanyika ili kuibua yale waliyofanikisha katika maisha yao.

Shirika la Tusonge pamoja na watendaji wote wanajivunia na kuguswa na hisia mbalimbali za mabadiliko chanya ambayo wadau wa mradi huu wamejitokeza kuishirikisha jamii kwa upana wake. Tunaamini huu ni mwanzo wa kuisaidia kuifanya jamii ielewe yale yanayotendeka katika jamii yetu na pia kuwahamasisha wanawake na vijana wa makundi mengine ya pembezoni kuweza kujiunga na jitihada hizi. Aidha tunakaribisha wadau wote wa maendeleo kuweza kutushauri na wale watakaopenda pia kusaidia michango ya hali na mali ili jitihada hizi ziweze kuwa endelevu.

Hebu jiunge na Toleo la NGUVU yetu la tatu kusikia shuhuda hizi mbalimbali.

Ahsanteni sana furahia kusoma shuhuda hizi.



Aginatha Rutazaa

MKURUGENZI MTENDAJI

Halima Mvumo, ni mjasiriamali wa soko la Maimoria, natokea Kata ya Majengo kikundi namba mbili Miembeni. Nilifanikiwa kujiunga na VICOBA mwaka 2011. Japokuwa kulikuwa na VICOBA vya aina nyingi Kata ya Majengo niliamua kujiunga na VICOBA vilivyoanzishwa na TUSONGE kwani niliviona ni vya tofauti sana kwa kuwa tulifanikiwa kupata elimu mbalimbali kama vile haki za binadamu, jinsia, uongozi, UKIMWI na Ujasiriamali.

Mafunzo hayo yalinipa ujasiri sana wa kutunisha mtaji wangu kwani nilianza kwa kukopa shilingi 380,000/= ukiwa ni mtaji wangu wa kwanza, mwaka 2012. Baada ya hapo niliweza kuendesha biashara yangu na kurejesha kwa wakati kulingana na sheria za kikundi zinavyoelekeza. Mwaka 2013 nilifanikiwa kuchukua mkopo mara mbili, mwanzo wa mwaka nilichukua shilingi 3,000,000/= na mwisho wa mwaka nilifanikiwa kuchukua shilingi 6,000,000/=. Nimeweza kupiga hatua katika biashara yangu kwa sasa naweza kununua beli za viatu kutoka mkoa wa Dar-es salaam na kuja Moshi bila kupitia mgongo wa wafanyabiashara wenye mitaji mikubwa.

Pia nimeweza kufungua akaunti yangu binafsi na kuweza kulipia mzigo wa viatu kupitia Benki. Hii inarahisisha shughuli zangu kufanyika kwa haraka, lakini pia kwa usalama zaidi wa fedha zangu.

Mwaka 2014, Majengo tumepata bahati ya kuanza kufanya biashara kama timu ya wajasiriamali wa Moshi Manispaa kupitia muundo wa mtandao tulioanzisha baada ya mafunzo ya TUSONGE na kujiita MTAWAMO - Mtandao wa Wajasiriamali Manispaa ya Moshi. Kutokana na mimi kujiunga kwenye mtandao huu yapo mambo mengi ambayo kwa kudhamiria kwa pamoja tunaweza kufanya mambo mazuri ya tofauti. Yapo maono, mbali mbali ambayo sisi kama wana mtandao tutaweza kuyafanya:

Kuwa na mradi wa pamoja: Tukifanikiwa kuanzisha mradi wa pamoja itasaidia kufanikisha mahitaji

TUSONGE - CDO NGUVU yetu

Oktoba-Desemba 2014 Toleo la 3 uk. 2

mbalimbali ya jamii na pia faida itakayopatikana sisi kama wadau wa mtandao huu tutagawana faida.

Nikiwa kama mama niliyevutiwa sana na MTAWAMO nimejifunza kuwa TUSONGE ina matarajio ya Mradi kuwa endelevu na kumilikiwa na jamii yenyewe.

"Naishukuru sana Tusonge kwa ujasiri iliyonijengea nimeweza kuongeza mtaji wangu na kujiamini kama mwanamke katika kuhimili ushindani wa biashara sokoni"

Sambamba na hilo tunategemea kuwa MTAWAMO tunayo mianya mingi itakayotusaidia kuwa na elimu endelevu. Kwa mfano kuwa karibu na wataalamu wa miradi kutoka serikalini na kutupatia elimu ya ujasiriamali.

MTAWAMO itasaidia kupunguza majukumu yaliyokuwa yakifanywa na mjasiriamali mmoja mmoja. Hii ni kwa sababu mradi unatarajiwa kuanzishwa hivi karibuni utaajiri muuzaji mwenye uelewa mzuri wa kimahesabu na sisi wanamtandao na viongozi wa MTAWAMO kulingana na katiba yetu itatusaidia kuitisha vikao vya kila mwezi na vya dharura ili kuweza kupata taarifa ya mapato na matumizi ya mradi ulioanzishwa, kushirikishana changamoto na kupendekeza ni nini kifanyike ndani ya huu umoja wetu. Demokrasia imekuwa ni nguzo muhimu sana katika uongozi na maamuzi yetu.

Kupitia TUSONGE nimeimarika na kujiamini Kiuongozi ndani na nje ya familia yangu. Kupitia uchaguzi wa viongozi uliofanywa na Wanamtandao Wajasiriamali,

Jane Lyimo, ni mjasiriamali wa duka Kata ya Msaranga. Nilifanikiwa kujiunga na VICOBA Mwaka 2012. Hadi kufikia hivi sasa nimekuwa na mabadiliko makubwa kwani nilipata elimu ya ujasiriamali, haki za binadamu, uongozi, jinsia, ukimwi afya ya uzazi na lishe.

Elimu ya ujasiriamali imenisaidia kumiliki biashara yangu mwenyewe. Pia elimu niliyopata kuhusu haki za binadamu imenisaidia kushiriki katika maamuzi ndani ya jamii ninayoishi. Kihistoria na kijadi, wanawake

"Mimi ni Mwenyekiti wa VICOBA Kata ya Msaranga na Mfuatiliaji na Mtathimini wa kazi za TUSONGE ngazi ya Kata hivyo shughuli hii imenipa ujasiri mkubwa sana wa kuweza kutatua changamoto wanazokua nazo wajasiriamali wa Kata ya Msaranga

wengi katika Kijijini hapa, wamekuwa hawana fursa kusimama na kuzungumza mbele ya hadhara na ya wanaume. Mawazo na sauti zao hazikusikilizwa. Mfumo huu dume umepungua kwa kiasi kikubwa sana baada ya mradi wa TUSONGE. kutokana na uelewa wa haki za binadamu kuongezeka wanawake wengi wameingia katika uongozi, pamoja na mimi nimeweza kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa kikundi na pia mwenyekiti wa VICOBA kata ya Msaranga na pia ni mfuatiliaji na mtathimini wa kazi za TUSONGE ndani ya jamii.

Shughuli ya ufuatiliaji binafsi nimeipenda kwa kuwa imeongeza ujasiri kwangu. Hii ni kutokana na kuwa na ujasiri wa kuuliza wajasiriamali mafanikio waliyoyapata, changamoto wanazokutana nazo na kuwapa ushauri. Nafasi hii ya ufuatiliaji imeniwezesha pia kuhimiza uaminifu kwa wajasiriamali ikiwemo kuchukua mkopo na kurejesha kwa wakati. Pia ninahamasika kuona mabadiliko ya kazi zetu ndani ya jamii kwa ajili ya huu mradi wa TUSONGE.

Timu ya ufuatiliaji shirikishi kata ya Msaranga ina wajumbe 15 ambao tunasaidiana kufuatilia. Kila mwezi tumekuwa na kikao cha kujadili maendeleo ya

TUSONGE - CDO NGUVU yetu

Oktoba-Desemba 2014 Toleo la 3 uk. 3

kubwa tunatoa taarifa TUSONGE kwa ajili ya ushauri zaidi. Kazi hii ni ya kujitolea tu na tunafurahia kuona wajasiriamali wameongezeka kutoka vikundi 3 hadi kufikia vikundi 10, na idadi ya walengwa 300 ndani ya kata ya Msaranga. TUSONGE imesaidia kupunguza umasikini na hali ya utegemezi ndani ya familia.

Mafanikio mengine ya Jane ni:

- Milo ya nyumbani imebadilika kwani familia yangu imeweza kula milo mitatu kwa siku ukilinganisha na miaka iliyopita.
- Mahitaji ya muhimu kama malazi, mavazi na hata nimeweza kuwa na nishati ya maji na umeme
- Biashara yangu imekuwa kwa kiasi kikubwa na kupanuka kiasi cha kuongeza jokofu, na majiko sanifu ili kutunza mazingira.

Naitwa **Efgenia Kimaro** ni kijana wa kike mjasiriamali katika kata ya Biriri na mkazi wa kata hii.

"Elimu niliyopata toka TUSONGE imenisaidia kuongeza kipato changu

Umri wangu ni miaka 26 nafurahi kupata nafasi ya kujiunga na TUSONGE kama mwanakikundi. Kikundi changu ni namba moja Biriri. Nimefanikiwa kujiunga na kikundi cha VICOBA Mwaka huu wa 2014. Kikundi kimefadhiliwa na shirika la TUSONGE nimependa kuwepo kwenye kikundi kwa sababu nimewezeshwa mafunzo ya ujasiriamali na kufanikiwa kupanga malengo yangu kibiashara. kutokana na elimu husika na nikizingatia yote niliyoweza kufahamu, nitatunisha mtaji wangu ambao nilivyoanza kipato changu kilikuwa cha chini sana kwa sasa kitapanda.

Shirika la TUSONGE kama lilivyoweza kujitambulisha limeweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali na bado wanaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa awamu tofauti. Mimi nimependa sana mafunzo ya ujasiriamali kutokana na jinsi walivyoweza kutuunganisha sisi wanajamii ambao kuanzia mwanzo hatukuweza kushirikiana nakufanya jambo kubwa kama hili la TUSONGE kutuanzishia wazo la pamoja la kukusanya hisa za pamoja na kukopeshana.

Jina langu ni **Godfrey Mungure** ni mjasiriamali niliye bahatika kujiunga na kikundi hiki cha wajasiriamali cha Biriri kilichoanzishwa na Shirika la TUSONGE mwishoni mwa mwezi Mei 2014. Umri wangu ni miaka 26. Furaha niliyonayo ni mwamko wa elimu niliyoipata.

"Shirika la TUSONGE limenisaidia sana kuona mapungufu yangu. Baada ya kupata mafunzo ya namna ya kuweka kumbukumbu zangu za biashara"

Mimi ni mjasiriamali kwenye duka la rejareja niliyefanya biashara pasipo kuweka kumbukumbu zangu, kwa sasa nimefunguka na nitafanya kazi yangu nikitegemea kujua faida na hasara zinazojitokeza mapema kutokana na mtiririko wa mahesabu ya kila siku.

Shirika la TUSONGE limenisaidia sana kuona mapungufu yangu yaliyosababisha kupata mafanikio mazuri japo nilijitahidi sana kuwa mwangalifu wakati mwingine nilishindwa kwa kusahau wadeni wangu niliokuwa siweki kumbukumbu zao. Nitatumia vitabu vyote vya kumbukumbu kama nilivyofundishwa.

Ninao uwezo wa kutambua haraka sana faida na hasara kwa kupitia mfumo huu wa kuweka kumbukumbu sahihi za mahesabu yangu. Vijana wengi tunapenda kutumia sana bila kujua ni nini tulichozalisha. **ASANTENI TUSONGE**

Jina langu ni **Gema Abel** nafanya biashara ya kuuza nguo za mitumba. Nimependa kujiunga kwenye kikundi cha jamii ili niweze kushirikiana na wenzangu kuweza kupata mkopo na kupanua biashara yangu.

Kwa sasa nilichopanga kutokana na mkopo wangu nitanunua mahindi kwa bei nafuu kipindi hiki cha mavuno baada ya miezi mitatu au minne nitauza kwa bei ya juu zaidi faida nitakayopata natarajia kununua kuku wa mayai kuendelea kuboresha ujasiriamali wangu

TUSONGE - CDO

NGUVU yetu

Oktoba-Desemba 2014

Toleo la 3 uk. 3

"TUSONGE wamenipa elimu inayonijengea ujasiri wa kufanya biashara. Mradi huu ni kinga ya kutusaidia sisi wasichana wadogo kutotumbukia kwenye mitego ya mahusiano yasiyo salama....."

TUSONGE wamenipa elimu inayonijengea ujasiri wa kufanya biashara,na sasa najitahidi kuweza kutumia elimu hii kwa uangalifu ili niweze kufanikiwa na malengo yangu yaweze kukamilika.

Wasichana wengi tunatumbukia katika mitego ya mahusiano ambayo si salama kwa kuwa tunakuwa na changamoto za kipato. Naamini mradi huu ni kinga ya kutusaidia hasa wanawake wadogo kiumri.

Loyce Christian nimejiunga na kikundi kilichoanzishwa na TUSONGE, ninatarajia kushiriki vyema kwenye mafunzo ya ujasiriamali yanayoendelea nikilenga kupata mkopo utakao nisaidia katika ujasiriamali wangu. Kwa kipindi cha mwanzo nilijiingiza kwenye ujasiriamali wa kilimo kutokana na nguvu yetu wanakikundi kutunisha mitaji yetu wenyewe naamini nitakuwa na mabadiliko makubwa zaidi.

Erick Maiko ni kijana mwenye umri wa miaka 22 sijaoa ninaishi kata ya Msaranga. Nilifanikiwa kujiunga na VICOBA vinavyosimamiwa na TUSONGE mwezi wa tano mwaka huu 2014. Kwa kweli nina kila sababu ya kuzungumza furaha niliyo nayo moyoni kuhusu shirika hili la TUSONGE. Hii ni kwa sababu mwanzoni, Msaranga ilikuwa na vikundi 3 vya watu wazima ambapo hakukuwepo na kikundi cha vijana. Mwaka 2014 TUSONGE iligundua umuhimu wa kuwahusisha vijana katika vikundi vya ujasiriamali ili waweze kupata mafunzo na kujikwamua kiuchumi.
Wawezeshaji kutoka TUSONGE walitupa taarifa kuwa

Vikundi vipya vianzishwe mwaka huu wa 2014 ikiwemo vikundi viwili vya vijana na vikundi vitano vya watu wazima. Hii ni kwa sababu shirika la TUSONGE linatumia muongozo kutoa huduma ya elimu katika jamii na pia waliona kuwa ili mradi kuwa endelevu ni vema kutoa elimu kwa vijana. Kata ya Msaranga tunategemea kupata mafunzo ya ujasiriamali kuanzia mwaka ujao 2015. Hadi kufikia hivi sasa vikundi 7 vimeongezeka kata ya Msaranga na sasa tuna jumla ya vikundi kumi 10. Tunaendelea kununua hisa, kutoa mfuko wa jamii na kuchukua mkopo na pia tunaendelea kurejesha mkopo kwa wakati huku tukiheshimu katiba yetu ya vikundi.

Hata hivyo mimi nimefanikiwa kuchukua mkopo kwenye kikundi chetu cha vijana nikaweza kununua mashine ya kupukuchua mahindi iliyogharimu fedha za kitanzania shilingi 1,200,000/=. Mashine hii imekuwa msaada mkubwa sana ndani ya kata yetu ya Msaranga na maeneo ya jirani kwani walio wengi ni wajasiriamali ambao kila wakati wanafanya biashara. Hivyo basi badala ya kutumia mikono kupukuchua mahindi,na kulipa fedha nyingi na muda mrefu wa vibarua wanatumia mashine yangu na kulipia. Kwa siku moja ninaweza kuingiza kiasi cha shilingi laki moja 100,000tsh. Kwa mtu mmoja analipa shilingi 30,000/= Vijana tunatamani sana tupate mafunzo ya ujasiriamali kutoka TUSONGE kwani uelewa tulionao kwa sasa ni mdogo sana, tunaamini kuanzia mwaka ujao tutaweza kuendesha biashara zetu vizuri na

Mjasiriamali Erick Maiko akiendesha mashine

kutambua namna ya kupata faida na hasara. Mungu awabariki sana TUSONGE Kwa kutukumbuka vijana kwani tulikuwa hatuna mwelekeo lakini sasa tumegundua umuhimu wa kujiunga na VICOBA.

VIJANA NI TEGEMEO LA LEO NA KESHO MIRADI ITUPE KIPAUMBELE KWANI TUNAWEZA NA PIA TUNAZO NGUVU ZA KUTOSHA.

MALENGO YA BAADAYE

- ✓ Tusonge inakususdia kuanzaisha Mradi wa masuala ya Haki za watoto na Vjana ili kuwa na uendelevu wa jitihada za kuheshimu usawa wa masuala ya kiuchumi katika jamii zetu.

- ✓ Kupanua wigo wa kutandaa na kushirikiana na wadau wengine wenye nia njema ya kukuuza maendeleo ya jamii

- ✓ Kushawishi na kuhimiza mabadiliko potofu na kandamizi yanyorudisha nyuma jitihada za wajasiriamali.

- ✓ Kuibua mikakati ya kuwasaidia zaidi wanawake wenye mahitaji maalumu kama wale wanaoishi na ulemavu kwenye eneo la kiuchumi kwani pia wanaweza.

TOLEO HILI LIMETOLEWA KWA MSAADA WA:

- Wafadhili wa Mradi wa TUSONGE Mkate kwa Dunia (Bread for the World Development Ujerumani)